# RosettaStone®

## KISWAHILI

レベル 1
スワヒリ語

Stufe 1
SWAHILI

Level 1
SWAHILI

단계 1
스와힐리어

Livello 1
SWAHILI

Nivel 1
SWAHILI

1 级
斯瓦希里语

Nível 1
SUAÍLE

Niveau 1
SWAHILI



## Course Content

Contenido del curso

Contenu du cours

Kursinhalt

Contenuto del corso

Conteúdo do curso

コース内容

코스 컨텐트 북

课文

CCB-KIS-L1-1.0 - 159397

ISBN 978-1-61716-457-6

All information in this document is subject to change without notice. This document is provided for informational purposes only and Rosetta Stone Ltd. makes no guarantees, representations or warranties, either express or implied, about the information contained within the document or about the document itself. Rosetta Stone®, Language Learning Success™, and Dynamic Immersion® are trademarks of Rosetta Stone Ltd.
Copyright © 2011 Rosetta Stone Ltd. All rights reserved.

Printed in the United States of America.

Rosetta Stone
Harrisonburg, Virginia USA
T (540) 432-6166 • (800) 788-0822 in the USA and Canada
F (540) 432-0953
RosettaStone.com

# RosettaStone®

# KISWAHILI

| | | |
|---|---|---|
| レベル 1<br>スワヒリ語 | Stufe 1<br>SWAHILI | Level 1<br>SWAHILI |
| 단계 1<br>스와힐리어 | Livello 1<br>SWAHILI | Nivel 1<br>SWAHILI |
| 1 级<br>斯瓦希里语 | Nível 1<br>SUAÍLE | Niveau 1<br>SWAHILI |

## Course Content

Contenido del curso

Contenu du cours

Kursinhalt

Contenuto del corso

Conteúdo do curso

**コース内容**

코스 컨텐트 북

**课文**

# Yaliyomo


**Misingi ya Lugha**

1.1 Somo Kuu ........ 1
1.2 Somo Kuu ........ 3
1.3 Somo Kuu ........ 5
1.4 Somo Kuu ........ 8
1.5 Mazingatio ........ 12

**Salamu na Utambulisho**

2.1 Somo Kuu ........ 12
2.2 Somo Kuu ........ 15
2.3 Somo Kuu ........ 17
2.4 Somo Kuu ........ 20
2.5 Mazingatio ........ 23

**Kazi na Shule**

3.1 Somo Kuu ........ 24
3.2 Somo Kuu ........ 26
3.3 Somo Kuu ........ 28
3.4 Somo Kuu ........ 31
3.5 Mazingatio ........ 33

**Kununua**

4.1 Somo Kuu ........ 34
4.2 Somo Kuu ........ 36
4.3 Somo Kuu ........ 39
4.4 Somo Kuu ........ 41
4.5 Mazingatio ........ 43

**Alfabeti ........ 45**

**Faharasa ........ 46**

# 1.1 Somo Kuu

01 Habari?
Nzuri.
Habari?
Nzuri.

02 msichana
mvulana
mvulana
msichana

03 msichana
mvulana

04 Msichana anakula.
Msichana anakunywa.
Mvulana anakula.
Mvulana anakunywa.

05 Msichana anakunywa.
Mvulana anakunywa.
Msichana anakula.
Mvulana anakula.

06 mwanamke
mwanamume
mwanamke
mwanamume

07 mwanamke
mwanamume

08 Mwanamke anakunywa.
Mwanamume anakula.
Mwanamke anakula.
Mwanamume anakunywa.

09 Mwanamume anakula.
Mwanamke anakula.
Msichana anakula.
Mvulana anakula.

10 Mwanamume anakula.
Msichana anakunywa.
Mwanamume anakunywa.
Msichana anakula.

11 Msichana anakimbia.
Mvulana anakimbia.
Mwanamume anakimbia.
Mwanamke anakimbia.

12 Msichana anasoma.
Mvulana anasoma.
Mwanamume anasoma.
Mwanamke anasoma.

13 Mwanamke anakimbia.
Mwanamke anasoma.
Mwanamke anakunywa.
Mwanamke anakula.

14 Mvulana anakimbia.
Mvulana anakula.
Mvulana anakunywa.
Mvulana anasoma.

15 Msichana anakunywa.
Wasichana wanakunywa.
Mvulana anakula.
Wavulana wanakula.

16 Mwanamume anakunywa.
Wanaume wanakunywa.
Msichana anakimbia.
Wasichana wanakimbia.

17 Mwanamke anakula.
Wanawake wanakula.
Mvulana anasoma.
Wavulana wanasoma.

18 wavulana
wasichana
wanaume
wanawake

19 Wanaume wanasoma.
Wanawake wanasoma.
Wanaume wanakimbia.
Wanawake wanakimbia.

# 1.1 Inaendelea

20 Msichana anasoma.
Wanawake wanasoma.
Mwanamke anasoma.
Wasichana wanasoma.

21 Wavulana wanakula.
Wasichana wanakimbia.
Wanawake wanakunywa.
Wanaume wanasoma.

22 Anakimbia.
Anakula.
Anakunywa.
Anasoma.

23 Anakimbia.
Anakunywa.
Wanakula.
Wanasoma.

24 Anakimbia.
Anakimbia.
Wanakimbia.

25 Anapika.
Anapika.
Wanapika.

26 Wavulana wanaogelea.
Msichana anaogelea.
Mwanamume anaogelea.
Wanawake wanaogelea.

27 Mwanamume anapika.
Wanaume wanapika.
Mwanamume anakula.
Wanaume wanakula.

28 Mwanamke anakimbia.
Mwanamke anaogelea.
Wanawake wanakimbia.
Wanawake wanaogelea.

29 Anaogelea.
Anakimbia.
Anapika.
Anakula.

30 Anaandika.
Anaandika.
Wanaandika.

31 Wanakula.
Wanapika.
Wanaogelea.
Wanaandika.

32 Wasichana wanasoma.
Msichana anasoma.
Wasichana wanaandika.
Msichana anaandika.

33 Anasoma.
Anakunywa.
Anaandika.
Anakula.

34 Anakunywa.
Anakula.
Anakunywa.
Anakula.

35 Kwaheri.
Kwaheri.

## 1.2 Somo Kuu

01 Habari?
Nzuri.

02 sandiwichi
sandiwichi
sandiwichi
yai
yai
tofaa

03 mkate
mkate
mkate
kahawa
kahawa
maziwa

04 sandiwichi
yai
tofaa
mkate
kahawa
maziwa

05 msichana na mwanamke
mvulana na mwanamume
sandiwichi na mkate

06 mwanamume na mwanamke
wali na tofaa
mkate na maji

07 Mvulana anakunywa maziwa.
Mwanamke anakunywa kahawa.
Mvulana na mwanamume wanakunywa maji.
Msichana anakula mkate.
Mwanamume anakula yai.
Mwanamume na mwanamke wanakula wali.

08 Anakula tofaa.
Anakula wali.
Wanakula mayai.
Wanakula sandiwichi.

09 Wanakula mayai.
Wanakula sandiwichi.
Anakula wali.
Anakunywa maji.

10 mbwa
mbwa
mbwa
paka
paka
farasi

11 gari
gari
gari
gazeti
gazeti
baiskeli

12 mbwa
paka
farasi
gari
gazeti
baiskeli

13 Mwanamume anaendesha gari.
Mwanamke anaendesha gari.
Mvulana anatembea.
Msichana anatembea.

14 Mwanamume anakimbia.
Mwanamke anatembea.
Msichana anakimbia.
Mvulana anatembea.

15 Wanakula matofaa.
Anaendesha gari.
Wanasoma gazeti.
Anasoma kitabu.

16 Mvulana ana paka.
Mwanamke ana mbwa.
Wasichana wana farasi.

17 Ana gari.
Ana sandiwichi.
Wana gazeti.

18 Mvulana ana vitabu.
Msichana ana samaki.
Mwanamume na mwanamke wana kalamu.

## 1.2 Inaendelea

19 kitabu
kalamu
samaki

20 Amelala.
Amelala.
Wamelala.

21 Samaki anaogelea.
Paka amelala.
Mbwa anakula.
Farasi anakimbia.

22 Wanaogelea.
Wanasoma.
Wanatembea.
Wamelala.

23 Watoto wanakunywa.
Watu wazima wanakula.
Watoto wanaogelea.
Watu wazima wanakimbia.

24 Mtoto anakimbia.
Watoto wanakimbia.
Mtu mzima anasoma.
Watu wazima wanasoma.

25 Mwanamume anaendesha gari.
Mvulana haendeshi gari.
Mwanamke anaendesha gari.
Msichana haendeshi gari.

26 Watu wazima wanapika.
Watu wazima hawapiki.
Watoto wanaandika.
Watoto hawaandiki.
Mwanamke anaendesha gari.
Mwanamke haendeshi gari.

27 Wanaogelea.
Hawaogelei.
Amelala.
Hajalala.

28 Hawapiki, wanakula.
Wanapika, hawali.
Hatembei, anakimbia.
Anatembea, hakimbii.

29 Wanawake wana wali.
Wanawake hawana wali.
Mvulana ana kalamu.
Mvulana hana kalamu.

30 Mvulana ana maziwa.
Mvulana hana maziwa.
Wasichana wana baiskeli.
Wasichana hawana baiskeli.

31 Mbwa anakimbia.
Mbwa hakimbii.
Wavulana wana maji.
Wavulana hawana maji.

32 Hii ni nini?
Hili ni tofaa.
Hii ni nini?
Hili ni gazeti.
Huyu ni nani?
Huyu ni mbwa.
Huyu ni nani?
Huyu ni farasi.

33 Huyu ni nani?
Huyu ni paka.
Hii ni nini?
Hii ni baiskeli.

34 Hii ni nini?
Hili ni yai.
Huyu ni nani?
Huyu ni samaki.
Hii ni nini?
Hii ni kalamu.

35 Je, amelala?
Ndiyo, amelala.
Je, amelala?
Hapana, hajalala.

36 Je, mbwa anaogelea?
Ndiyo.
Je, farasi anaogelea?
Hapana.

37 Je, anasoma gazeti?
Hapana.
Je, anasoma kitabu?
Ndiyo.

38 Je, anakula tofaa?
Hapana.
Je, anakula tofaa?
Ndiyo.

39 Kwaheri.
Kwaherini.
Kwaheri.
Kwaherini.

## 1.3 Somo Kuu

01 Habari?
Nzuri.

02 tofaa
yai
gari
matofaa
mayai
magari

03 samaki
paka
farasi
samaki
paka
farasi

04 baiskeli
kalamu
kitabu
mpira
baiskeli
kalamu
vitabu
mipira

05 samaki
magari
kalamu
vitabu

06 nyeupe
nyeupe
nyeupe
nyeusi
nyeusi
nyekundu

07 buluu
buluu
buluu
kijani
kijani
manjano

## 1.3 Inaendelea

08 buluu
nyeupe
kijani
nyeusi
nyekundu
manjano

09 Yai ni jeupe.
Gari ni jeupe.
Baiskeli ni nyeupe.
Kalamu ni nyeupe.
Paka ni mweupe.
Farasi ni mweupe.
Kitabu ni cheupe.
Mpira ni mweupe.

10 Mpira ni mwekundu.
Tofaa ni jekundu.
Mbwa ni mweupe.
Kalamu ni nyeupe.
Kitabu ni cheusi.
Gari ni jeusi.

11 Gari ni la kijani.
Tofaa ni la kijani.
Baiskeli ni ya kijani.
Kalamu ni ya kijani.
Samaki ni wa kijani.
Kitabu ni cha kijani.
Mpira ni wa kijani.

12 Gari ni la manjano.
Samaki ni wa manjano.
Yai ni la buluu.
Mpira ni wa buluu.
Kitabu ni cha kijani.
Baiskeli ni ya kijani.

13 Yai ni jeupe.
Kalamu ni ya kijani.
Samaki ni wa buluu.
Yai ni la manjano.
Kalamu ni nyekundu.
Samaki ni mweusi.

14 Mbwa ni mweusi.
Mbwa ni mweupe.
Paka ni mweusi.
Paka ni mweupe.

15 Mayai ni mekundu.
Magari ni mekundu.
Baiskeli ni nyekundu.
Kalamu ni nyekundu.
Samaki ni wekundu.
Vitabu ni vyekundu.
Mipira ni miekundu.

16 Paka ni weusi.
Mipira ni mieusi.
Farasi ni weupe.
Baiskeli ni nyeupe.
Vitabu ni vyekundu.
Magari ni mekundu.

17 Magari ni ya manjano.
Matofaa ni ya manjano.
Baiskeli ni za manjano.
Kalamu ni za manjano.
Samaki ni wa manjano.
Vitabu ni vya manjano.
Mipira ni ya manjano.

18 Mayai ni ya buluu.
Samaki ni wa buluu.
Kalamu ni za kijani.
Matofaa ni ya kijani.
Baiskeli ni za manjano.
Mipira ni ya manjano.

19 Baiskeli ni nyeusi.
Mipira ni miekundu.
Magari ni ya manjano.
Baiskeli ni za buluu.
Mipira ni ya kijani.
Magari ni meupe.

20 mwezi
jua
anga
mti
ua
nyasi

21 Nyasi ni za kijani.
Anga ni ya buluu.
Mwezi ni mweupe.
Jua ni la manjano.
Ua ni jekundu.

22 Jua ni la manjano.
Tofaa ni la manjano.
Anga ni ya buluu.
Yai ni la buluu.

23 Mwezi ni mweupe.
Gari ni jeupe.
Nyasi ni za kijani.
Mpira ni wa kijani.

24 Ua ni dogo.
Yai ni dogo.
Maua ni madogo.
Mayai ni madogo.

25 Maua ni makubwa.
Vitabu ni vikubwa.
Samaki ni mkubwa.
Yai ni kubwa.

26 Mbwa ni mkubwa.
Mbwa ni mdogo.
Maua ni makubwa.
Maua ni madogo.

27 daktari
mwalimu
polisi
wanafunzi

28 Yeye ni mwanafunzi.
Yeye ni mwanafunzi.
Wao ni wanafunzi.

29 Yeye ni polisi.
Yeye ni mwalimu.
Yeye ni daktari.
Wao ni wanafunzi.

30 Mimi ni mvulana.
Mimi ni msichana.
Mimi ni mwanamume.
Mimi ni mwanamke.

31 Mimi ni mwalimu.
Mimi si mwalimu.
Mimi ni daktari.
Mimi si daktari.
Mimi ni mwanafunzi.
Mimi si mwanafunzi.

32 Nina kitabu cha kijani.
Nina kitabu cha manjano.
Nina kitabu chekundu.

33 Una kitabu cha kijani.
Una kitabu cha manjano.
Una kitabu chekundu.

34 Mimi ni mwanafunzi.
Wewe ni mwalimu.
Wewe ni polisi.
Wewe ni daktari.

35 Je, wewe ni daktari?
Ndiyo, mimi ni daktari.
Je, wewe ni daktari?
Hapana, mimi si daktari.

36 Unakunywa nini?
Ninakunywa maji.
Unakula nini?
Ninakula wali.

37 Una nini?
Nina sandiwichi.
Una nini?
Nina kalamu.

## 1.3 Inaendelea

38 Mimi ni mwalimu.
Sisi ni walimu.
Mimi ni msichana.
Sisi ni wasichana.

39 Sisi ni wasichana.
Sisi ni wavulana.
Sisi ni polisi.
Sisi ni madaktari.

40 Nina baiskeli nyekundu.
Tuna baiskeli za kijani.
Nina matofaa mekundu.
Tuna matofaa ya kijani.

41 Nina maua mekundu.
Una maua mekundu.
Ana maua mekundu.
Ana maua mekundu.
Tuna maua mekundu.
Wana maua mekundu.

42 Mwanamume anafanya nini?
Mwanamume anapika.
Mwanamke anafanya nini?
Mwanamke anasoma.
Mvulana anafanya nini?
Mvulana anakimbia.

43 Daktari anafanya nini?
Daktari anaandika.
Polisi anafanya nini?
Polisi anaendesha gari.
Msichana anafanya nini?
Msichana anatembea.

44 Unafanya nini?
Ninaandika.
Unafanya nini?
Ninaendesha gari.

45 Kwaheri.
Kwaherini.
Kwaheri.
Kwaherini.

## 1.4 Somo Kuu

01 Habari?
Nzuri.

02 moja
mbili
tatu
nne
tano
sita

03 moja, mbili, tatu
sita, moja, tatu, tano, mbili
mbili, nne, sita
moja, mbili, tatu, nne, tano

04 gari moja
yai moja
mbwa wawili
kalamu mbili
baiskeli tatu
paka watatu

05 wavulana wanne
wanaume wanne
magazeti matano
vitabu vitano
wasichana sita
matofaa sita

06 Kuna samaki mmoja.
Kuna kitabu kimoja.
Kuna mwanamke mmoja.
Kuna yai moja.
Kuna mtoto mmoja.
Kuna simu ya mkononi moja.

07 Kuna samaki watano.
Kuna vitabu vitatu.
Kuna wanawake wanne.
Kuna mayai sita.
Kuna watoto wawili.
Kuna simu ya mkononi moja.

08 Kuna simu za mkononi mbili.
Kuna mipira mitatu.
Kuna kitanda kimoja.
Kuna funguo nne.

09 Kuna kikombe kimoja.
Kuna viti vinne.
Kuna meza mbili.
Kuna simu tatu.

10 Kuna simu ya mkononi moja.
Kuna simu za mkononi mbili.
Kuna meza moja.
Kuna meza mbili.

11 Kuna samaki wangapi?
Kuna samaki watatu.
Kuna funguo ngapi?
Kuna funguo nne.
Kuna polisi wangapi?
Kuna polisi wawili.
Kuna matofaa mangapi?
Kuna tofaa moja.

12 Kuna viti vingapi?
Kuna viti sita.
Kuna simu ngapi?
Kuna simu tano.
Kuna vitanda vingapi?
Kuna vitanda viwili.

13 bakuli
bakuli
bakuli
sahani
sahani
kikombe

14 Kuna mayai matatu.
Kuna mayai matano.
Kuna vikombe vinne.
Kuna vikombe sita.

15 Sahani tatu ni nyeupe.
Matofaa mawili ni ya kijani.
Ua moja ni jekundu.
Mabakuli manne ni ya buluu.

16 Kuna meza ngapi nyeupe?
Meza mbili ni nyeupe.
Kuna mipira mingapi miekundu?
Mpira mmoja ni mwekundu.
Kuna mabakuli mangapi ya manjano?
Mabakuli mawili ni ya manjano.
Kuna simu ngapi nyeusi?
Simu moja ni nyeusi.

17 viatu
viatu
viatu
shati
shati
suruali ndefu

18 koti
koti
koti
gauni
gauni
sketi

19 viatu
shati
suruali ndefu
koti
gauni
sketi

20 shati la buluu
shati jekundu
fulana ya kijani
fulana nyeusi

21 Mna vikombe vingapi?
Tuna vikombe vinne.
Mna sandiwichi ngapi?
Tuna sandiwichi tano.

22 Mna mabakuli mangapi?
Tuna mabakuli matatu.
Mna sahani ngapi?
Tuna sahani mbili.

## 1.4 Inaendelea

23 Nina maua ya manjano.
Una maua mekundu.
Tuna maua meupe.
Mna maua ya buluu.

24 Msichana amevaa fulana.
Mvulana hajavaa fulana.
Mwanamke amevaa viatu.
Mwanamume hajavaa viatu.

25 Mvulana amevaa suruali ndefu.
Msichana hajavaa suruali ndefu, amevaa sketi.
Wanaume wamevaa kofia.
Wanawake watatu wamevaa suruali ndefu. Mwanamke mmoja amevaa gauni.

26 Nimevaa viatu.
Nimevaa gauni.
Tumevaa kofia.
Tumevaa makoti.

27 Mwanamke amevaa gauni.
Mwanamke amevaa sketi.
Mwanamke amevaa suruali ndefu.
Mwanamke amevaa kofia.

28 Mwanamume ananunua kofia moja.
Mwanamke ananunua kofia mbili.
Mwanamume ananunua fulana tatu.
Mwanamke ananunua fulana nne.

29 Mwanamume amevaa koti.
Mwanamume ananunua koti.
Mwanamume amevaa kofia.
Mwanamume ananunua kofia.

30 Ninanunua sketi.
Nimevaa sketi.
Ninanunua suruali ndefu.
Nimevaa suruali ndefu.

31 Nani anakula?
Polisi anakula.
Nani anasoma?
Wanafunzi wanasoma.
Nani anakunywa?
Wanawake wanakunywa.
Nani anaandika?
Msichana anaandika.

32 Nani ana kofia?
Mwanamke ana kofia.
Nani ana mpira?
Mvulana ana mpira.
Nani ana vitabu?
Wasichana wana vitabu.
Nani ana gazeti?
Daktari ana gazeti.

33 Nani amevaa viatu?
Nimevaa viatu.
Nani amevaa kofia?
Tumevaa kofia.

34 Nani anatembea?
Tunatembea.
Nani anakimbia?
Tunakimbia.

35 Kuna miti mingapi?
Kuna miti mitatu.
Kuna miti mingapi?
Kuna miti minne.
Kuna mabakuli mangapi?
Kuna bakuli moja.
Kuna watoto wangapi?
Kuna watoto sita.

36 Hii ni nini?
Huu ni mkate.
Hii ni nini?
Hiki ni kitanda.
Hii ni nini?
Haya ni maji.
Hii ni nini?
Hii ni sahani.

37 Baiskeli hii ni ya manjano.
Baiskeli ile ni ya buluu.
Mpira huu ni wa kijani.
Mpira ule ni mwekundu.

38 Wavulana hawa wanatembea.
Wavulana wale wanatembea.
Wasichana hawa wanasoma.
Wasichana wale wanasoma.

39 Haya ni maji.
Ile ni kahawa.
Haya ni matofaa mekundu.
Yale ni matofaa ya kijani.

40 Mpira huu ni mwekundu. Mpira ule ni wa manjano.
Mpira huu ni wa manjano. Mpira ule ni mwekundu.
Magari haya ni meupe.
Magari yale ni mekundu.

41 Hii ni nini?
Huu ni mti.
Je, nyasi ni za kijani?
Ndiyo, nyasi ni za kijani.

42 Hii ni nini?
Hii ni baiskeli.
Kuna baiskeli ngapi?
Kuna baiskeli tatu.
Nani ana baiskeli?
Mwanamke ana baiskeli.
Je, ana baiskeli?
Ndiyo, ana baiskeli.

43 Hii ni nini?
Hii ni sandiwichi.
Kuna sandiwichi ngapi?
Kuna sandiwichi mbili.
Je, mnakula sandiwichi?
Ndiyo, tunakula sandiwichi.

44 Kuna funguo ngapi?
Kuna funguo nne.
Mnafanya nini?
Tunaandika.
Je, mna samaki?
Ndiyo, tuna samaki.
Je, farasi ni mweusi?
Hapana, farasi si mweusi.

45 Samahani.
Una nini?
Nina mbwa.
Samahani.
Unakunywa nini?
Ninakunywa kahawa.

46 Samahani.
Hii ni nini?
Hii ni sahani.
Samahani.
Wanakula nini?
Wanakula mayai.

47 Samahani.
Anakula nini?
Sijui.
Samahani.
Je, yeye ni daktari?
Sijui.

48 Samahani.
Anapika nini?
Sijui.
Samahani.
Unapika nini?
Ninapika wali.

49 Hii ni nini?
Huu ni mti.
Hii ni nini?
Sijui.

50 Habari?
Nzuri.
Kwaheri.
Kwaheri.

## 1.5 Mazingatio

01 Habari?
Nzuri.

02 Je, una mbwa?
Ndiyo, nina mbwa.

03 Unafanya nini?
Ninasoma.

04 Hii ni nini?
Hii ni kahawa.

05 Je, una kikombe?
Ndiyo, nina kikombe.

06 Una nini?
Nina mkate.

07 Mna nini?
Tuna matofaa.

08 Mbwa anafanya nini?
Mbwa anakula.

## 2.1 Somo Kuu

01 mwanamume na mbwa
mwanamke na mbwa wake
msichana na farasi
polisi na farasi wake

02 mwanamke na gari lake
mwanamke na paka wake
mwanamume na gari lake
mwanamume na paka wake

03 Wanakula sandiwichi zao.
Wanasoma gazeti lao.
Wanasoma magazeti yao.
Wanasoma kitabu chao.
Wanakula matofaa yao.

04 Wanasoma vitabu vyao.
Anasoma kitabu chake.
Anasoma kitabu chake.
Wanakula matofaa yao.
Anakula tofaa lake.
Anakula tofaa lake.

05 familia
familia
familia

06 familia
mwanamke na binti yake
mwanamume na mtoto wake wa kiume

07 familia
mvulana na baba yake
msichana na mama yake

08 mama
binti
baba
mtoto wa kiume

09 mtoto mchanga
mwanamke na mume wake
msichana na wazazi wake
wasichana wawili na wazazi wao

10 mwanamume na mke wake
mwanamke na watoto wake
baba na binti yake
wazazi na watoto wao wa kiume

11 mama na mtoto wake mchanga
baba na watoto wake
mume na mke wake
wazazi na binti yao

12 Baba na watoto wake wa kiume wanacheza.
Mama na binti zake wanacheza.
Mvulana na mbwa wake wanacheza.
Mwanamke na paka wake wanacheza.

13 Mtoto wa kiume hachezi. Baba yake anacheza.
Baba hasomi. Binti yake anasoma.
Watoto hawapiki. Baba yao anapika.

14 Nani anacheza?
Mvulana anacheza.
Nani amelala?
Mwanamke amelala.
Nani anakula?
Mwanamume anakula.
Nani anakunywa?
Mwanamke anakunywa.

15 Huyu ni mama yangu.
Huyu ni baba yangu.
Huyu ni mtoto wangu wa kiume.
Huyu ni binti yangu.
Hii ni baiskeli yangu.
Hiki ni kitanda changu.

16 Hii ni familia yangu.
Huyu ni baba yangu.
Huyu ni mama yangu.
Huyu ni dada yangu.
Huyu ni kaka yangu.

17 Mdogo wangu wa kiume anakimbia.
Kaka yangu anakula tofaa.
Mdogo wangu wa kike anacheza.
Dada yangu anasoma kitabu.

18 Mdogo wangu wa kiume anakunywa.
Kaka yangu anaandika.
Mdogo wangu wa kike anatembea.
Dada yangu anapika.

19 Huyu ni kaka yangu.
Huyu ni mdogo wangu wa kiume.
Huyu ni dada yangu.
Huyu ni mdogo wangu wa kike.
Huyu ni kaka yangu.
Huyu ni mdogo wangu wa kiume.
Huyu ni dada yangu.
Huyu ni mdogo wangu wa kike.

20 Yeye ni dada yangu.
Yeye ni rafiki yangu.
Yeye ni mdogo wangu wa kiume.
Yeye ni rafiki yangu.

21 Hawa ni dada zangu.
Hawa ni wadogo wangu wa kiume.
Wao si wadogo wangu wa kiume. Wao ni rafiki zangu.
Wao si dada zangu. Wao ni rafiki zangu.

22 Huyu ni rafiki yangu.
Hawa ni rafiki zangu.
Huyu ni mdogo wangu wa kiume.
Hawa ni wadogo wangu wa kiume.

23 Huyu ni mdogo wangu wa kike.
Hawa ni wadogo wangu wa kike.
Huyu ni mama yangu.
Hawa ni wazazi wangu.

24 Huyu ni mtoto wangu mchanga.
Hawa ni watoto wangu.
Huyu ni mama yangu.
Hawa ni watoto wangu wa kiume.
Huyu ni dada yangu.
Hawa ni wazazi wangu.

25 Huyu ni mtoto wetu wa kiume.
Huyu ni mtoto wangu wa kiume.
Huyu ni mama yetu.
Huyu ni mama yangu.
Hawa ni watoto wetu.
Hawa ni wazazi wetu.

# 2.1 Inaendelea

26 Baiskeli yake ni kubwa.
Baiskeli yake ni ndogo.
Baiskeli yao ni ya kijani.
Baiskeli yangu ni ya buluu.
Baiskeli yetu ni nyeusi.

27 Wewe ni rafiki yangu.
Wewe ni daktari wangu.
Wewe ni mke wangu.
Wewe ni mwalimu wangu.

28 Wewe ni mdogo wangu wa kiume.
Wewe ni dada yangu.
Wewe ni rafiki yangu.

29 Nyinyi ni walimu wangu.
Nyinyi ni rafiki zangu.
Nyinyi ni wazazi wangu.
Nyinyi ni kaka zangu.

30 Nyinyi ni wadogo wangu wa kiume.
Nyinyi ni wadogo wangu wa kike.
Wewe ni mdogo wangu wa kiume.
Wewe ni mdogo wangu wa kike.

31 Unafanya nini?
Ninapika.
Mnafanya nini?
Tunakula.
Unafanya nini?
Ninapika.
Mnafanya nini?
Tunakula.

32 Tuna watoto wawili wa kiume.
Tuna binti wanne.
Tuna mtoto wa kiume mmoja na binti watatu.

33 sita
saba
nane
tisa
kumi
kumi na moja
kumi na mbili
sifuri

34 tatu, mbili, moja, sifuri
sita, saba, nane, tisa, kumi
sita, nane, kumi, kumi na mbili
kumi na moja, sifuri, tisa, tano

35 kalamu saba
watoto wachanga saba
mayai manane
viti vinane
kofia tisa
matofaa tisa

36 sahani kumi
vikombe kumi
mabakuli kumi na moja
maua kumi na moja
mipira kumi na mbili
funguo kumi na mbili

37 Ana umri wa mwaka mmoja.
Ana umri wa miaka miwili.
Ana umri wa miaka mitatu.
Ana umri wa miaka minne.
Ana umri wa miaka mitano.
Ana umri wa miaka sita.
Ana umri wa miaka saba.
Ana umri wa miaka minane.

38 Ana umri gani?
Ana umri wa miaka sita.
Ana umri gani?
Ana umri wa miaka saba.

39 Una umri gani?
Nina umri wa miaka mitano.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka minne.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka kumi.

40 Ana umri gani?
Ana umri wa miaka kumi na mbili.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka mitano.
Ana umri gani?
Ana umri wa miaka tisa.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka tisa.

## 2.2 Somo Kuu

01 fleti
fleti
fleti
nyumba
nyumba
mlango

02 televisheni
televisheni
televisheni
redio
redio
kompyuta

03 kompyuta
kompyuta
laptopu
laptopu

04 fleti
mlango
nyumba
kompyuta
televisheni
redio

05 Laptopu ipo juu ya meza.
Redio ipo juu ya kiti.
Paka yupo juu ya televisheni.
Tofaa lipo juu ya laptopu.

06 Kompyuta imo garini.
Funguo zimo kiatuni.
Paka yumo kofiani.

07 Mwanamume yumo garini.
Mwanamume yupo juu ya gari.
Paka yumo nyumbani.
Paka yupo juu ya nyumba.

08 dirisha
dirisha
dirisha
choo
choo
sinki

09 sebule
sebule
sebule
jiko
jiko
bafu

10 sebule
bafu
jiko
dirisha
choo
sinki

11 Matofaa yamo bakulini.
Bakuli lipo juu ya meza.
Meza imo jikoni.
Jiko limo nyumbani.

12 Mvulana yumo nyumbani.
Msichana yumo fletini.
Familia imo nyumbani.
Mwanamke yumo fletini.

13 Mlango huu ni mkubwa.
Mlango huu ni mdogo.
Dirisha hili ni kubwa.
Dirisha hili ni dogo.

14 chumba cha kulala
chumba cha kulala
chumba cha kulala
chumba cha maakuli
chumba cha maakuli
bafu

15 Mwanamume yumo katika chumba cha maakuli.
Paka yumo katika chumba cha kulala.
Familia imo katika chumba cha maakuli.
Laptopu imo katika chumba cha kulala.

16 Jiko ni la kijani.
Chumba cha kulala ni cha kijani.
Bafu ni la kijani.
Sebule ni ya kijani.
Chumba cha maakuli ni cha kijani.
Nyumba ni ya kijani.

## 2.2 Inaendelea

17 Msichana na nyanya yake wamo katika chumba cha maakuli.
Mvulana na babu yake wamo bafuni.
Msichana na babu yake wanacheza.
Mvulana na nyanya yake wanapika.

18 Baba anamkumbatia mtoto wake wa kiume.
Mama anamkumbatia binti yake.
Mume anambusu mke wake.
Msichana anambusu kaka yake.

19 Ninamkumbatia mdogo wangu wa kike.
Ninamkumbatia mbwa.
Msichana anambusu mama yake.
Mtoto anambusu baba yake.

20 Anamkumbatia nyanya yake.
Anambusu mtoto wake.
Ninamkumbatia dada yangu.
Anambusu mume wake.

21 Ninampenda mama yangu.
Ninampenda mdogo wangu wa kiume.
Ninampenda mdogo wangu wa kike.
Ninampenda babu yangu.

22 Mke anampenda mume wake.
Wazazi wanawapenda watoto wao.
Mvulana anampenda babu yake.
Msichana anampenda mbwa wake.

23 Msichana anamkumbatia mdogo wake wa kike.
Mume anambusu mke wake.
Watoto wanampenda mama yao.
Ninampenda mtoto wangu mchanga.

24 Paka yupo chini ya meza.
Mbwa yupo chini ya shati.
Wavulana wapo chini ya kitanda.

25 Paka yupo juu ya meza.
Paka yupo chini ya meza.
Nipo juu ya kitanda.
Nipo chini ya kitanda.

26 Mwanamume yupo juu ya gari.
Mwanamume yumo garini.
Mwanamume yupo chini ya gari.

27 Msichana yupo juu ya kitanda.
Msichana yupo chini ya kitanda.
Mwanamume yupo juu ya gari.
Mwanamume yupo chini ya gari.

28 Wavulana wanatazama televisheni.
Mtoto anasikiliza.
Paka anamwangalia samaki.
Wazazi wanasikiliza.

29 Mwanamume anatazama televisheni.
Msichana anasikiliza redio.
Wazazi wanawaangalia watoto wao.
Mvulana na msichana wanamwangalia samaki.

30 Mwanamume anasikiliza redio.
Familia inatazama televisheni.
Msichana anamwangalia baba yake.

31 Mwanamume amesimama.
Mvulana amekaa.
Mwanamke amesimama.
Msichana amekaa.

32 Mama amekaa jikoni.
Binti amekaa sebuleni.
Mvulana amesimama sebuleni.
Baba amesimama jikoni.

33 Mwanamume amesimama.
Mwanamume amekaa.
Mwanamke amesimama.
Mwanamke amekaa.

34 Je, hiki ni kitabu chako?
Ndiyo, hiki ni kitabu changu.
Je, hii ni kofia yako?
Hapana, hii si kofia yangu.

35 Je, yeye ni dada yako?
Ndiyo, ni dada yangu.
Je, huu ni mpira wako?
Ndiyo, ni mpira wangu.

36 Funguo zangu ziko wapi?
Funguo zako zimo garini.
Koti langu liko wapi?
Koti lako lipo juu ya kiti.

37 Vitabu vyangu viko wapi?
Vitabu vyako vipo juu ya kiti.
Kikombe changu kiko wapi?
Kikombe chako kimo sinkini.

38 Je, yeye ni kaka yako?
Ndiyo, ni kaka yangu.
Gazeti langu liko wapi?
Gazeti lako lipo juu ya meza.

39 Viatu viko wapi?
Viatu vipo chini ya kitanda.
Gazeti liko wapi?
Gazeti lipo juu ya kitanda.

40 Vikombe viko wapi?
Vikombe vimo sinkini.
Sahani ziko wapi?
Sahani zimo sinkini.

## 2.3 Somo Kuu

01 Ninaishi kwenye fleti.
Ninaishi kwenye nyumba.
Tunaishi kwenye fleti.
Tunaishi kwenye nyumba.

02 Ninaishi kwenye nyumba.
Anaishi kwenye fleti.
Wanaishi kwenye nyumba.
Tunaishi kwenye fleti.

03 Unaishi wapi?
Ninaishi kwenye fleti hii.
Unaishi wapi?
Ninaishi kwenye fleti hii.

04 Roma
Roma
Roma
Paris
Paris
Mosko

05 Unaishi wapi?
Ninaishi Mosko.
Unaishi wapi?
Ninaishi Paris.

06 Mnaishi wapi?
Tunaishi Roma.
Mnaishi wapi?
Tunaishi Mosko.
Mnaishi wapi?
Tunaishi Paris.

07 nchi
nchi
nchi
jiji
jiji
daraja

08 bustani
bustani
bustani
barabara
barabara
daraja

# 2.3 Inaendelea

09 nchi
jiji
barabara
bustani
daraja

10 Msichana amekaa juu ya daraja.
Mwanamume amesimama katika barabara.
Wasichana wamesimama juu ya daraja.
Mwanamke amekaa katika bustani.

11 Barabara hii iko Paris.
Jiji hili liko Ufaransa.
Daraja hili liko New York.
Jiji hili liko Marekani.

12 Wanatoka Ufaransa.
Anatoka Ufaransa.
Anatoka Ufaransa.
Watoto hawa wanatoka Marekani.
Mwanamume huyu anatoka Marekani.
Mwanamke huyu anatoka Marekani.

13 Tunatoka Kenya.
Ninatoka Kenya.
Anatoka Tanzania.
Mnatoka Tanzania.

14 Uchina
Uchina
Uchina
Urusi
Urusi
Misri

15 Unatoka nchi gani?
Ninatoka Marekani.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Misri.
Mnatoka nchi gani?
Tunatoka Ufaransa.
Mnatoka nchi gani?
Tunatoka Uchina.

16 Brazili
Brazili
Brazili
Japani
Japani
Italia

17 Marekani
Japani
Kenya
Tanzania
Ninatoka Marekani.
Ninatoka Japani.
Ninatoka Kenya.
Ninatoka Tanzania.

18 Anatoka nchi gani?
Anatoka Japani.
Wanatoka nchi gani?
Wanatoka Kenya.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Marekani.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Tanzania.

19 Unatoka nchi gani?
Ninatoka Kenya.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Japani.

20 Unatoka nchi gani?
Ninatoka Marekani.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Tanzania.

21 Mvulana yupo karibu na nyumba.
Msichana yupo mbali na nyumba.
Mbwa yupo karibu na nyumba.
Farasi yupo mbali na nyumba.

22 Nyumba yangu ipo karibu na barabara.
Nyumba yangu ipo mbali na barabara.
Kiti kipo karibu na mlango.
Kiti kipo mbali na mlango.

23 Nipo karibu na mti.
Nipo mbali na mti.
Nipo karibu na daraja.
Nipo mbali na daraja.

24 Jina la nchi hii ni Italia.
Jina la nchi hii ni Japani.
Jina la nchi hii ni Misri.
Jina la nchi hii ni Urusi.

25 Japani ipo karibu na Uchina.
Japani ipo mbali na Brazili.
Italia ipo karibu na Ufaransa.
Italia ipo mbali na Brazili.

26 Habari?
Jina langu ni Anna.
Habari?
Jina langu ni David.
Habari?
Jina langu ni Sara.

27 Habari?
Nzuri.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni Robert.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni Lin.

28 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Maria.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni Ravi.

29 Habari?
Nzuri.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni Isabela.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni Laura.

30 Jina langu ni Mei.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

31 Jina langu ni Steve.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.
Jina langu ni Catherine.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

32 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Robert.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.
Kwaheri.
Kwaheri.

33 Unatoka nchi gani?
Ninatoka Marekani.
Na wewe unatoka nchi gani?
Ninatoka Urusi.

34 Habari?
Nzuri.
Jina lako ni nani?
Jina langu ni David.

35 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Akiko.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

36 Unatoka nchi gani?
Ninatoka Urusi.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Marekani.
Na wewe unatoka nchi gani?
Ninatoka Japani.

37 Habari? Jina langu ni Viktor.
Habari? Jina langu ni Lin.
Habari? Jina langu ni Isabela.
Habari? Jina langu ni Pierre.

38 Ninaishi Mosko, Urusi.
Ninaishi Beijing, Uchina.
Ninaishi Roma, Italia.
Ninaishi Paris, Ufaransa.

## 2.3 Inaendelea

39 Hiki ni chumba changu cha kulala.
Hili ni jiko langu.
Hiki ni chumba changu cha kulala.
Hili ni jiko langu.

40 Huyu ni mama yangu. Jina lake ni Mei. Anapika jikoni.
Huyu ni kaka yangu. Jina lake ni Vladimir. Amelala katika chumba cha kulala.
Huyu ni baba yangu. Jina lake ni Bertrand. Anakula katika chumba cha maakuli.
Huyu ni mdogo wangu wa kike. Jina lake ni Giulia. Anacheza katika bustani.

## 2.4 Somo Kuu

01 sweta
sweta
sweta
jinzi
jinzi
mkanda

02 suti
suti
suti
soksi
soksi
tai

03 sweta
tai
suti
soksi
mkanda
jinzi

04 Soksi zangu ni za kijivu.
Soksi zake ni za zambarau.
Sweta yangu ni ya zambarau.
Sweta yake ni ya kijivu.

05 Mwanamume mrefu amevaa tai.
Mwanamume mfupi amevaa sweta.
Mwanamke mrefu amevaa jinzi.
Mwanamke mfupi amevaa fulana.

06 Mwanamume mrefu amevaa suti nyeusi.
Mwanamume mfupi amevaa suti nyeusi.
Mwanamke mrefu amevaa suti ya kijivu.
Mwanamke mfupi amevaa suti ya kijivu.

07 Gauni langu ni la pinki.
Viatu vyangu ni vya kahawia.
Mkanda wangu ni wa pinki.
Tai yangu ni ya kahawia.

08 Suruali yake ndefu ni ya buluu.
Fulana yake ni ya kimachungwa.
Koti lake ni la buluu.
Gauni lake ni la kimachungwa.

09 Kofia yangu ni ya buluu.
Tai yangu ni ya kimachungwa.
Mkanda wangu ni wa kahawia.
Sweta yangu ni ya zambarau.

10 Mkanda ni wa pinki.
Nyumba ni ya kahawia.
Nyumba ni ya pinki.
Mkanda ni wa kahawia.

11 kijivu
zambarau
pinki
kahawia
kimachungwa
buluu
manjano
kijani

12 Nina nywele za kahawia.
Ana nywele za kahawia.
Tuna nywele za shaba.
Wana nywele za shaba.

13 Nina nywele nyekundu.
Mna nywele nyekundu.
Ana mvi.
Tuna mvi.

14 Mimi ni mrefu.
Nina nywele za kahawia.
Mimi ni mfupi.
Nina nywele nyekundu.

15 Ana nywele nyeusi.
Ana mvi.
Ana nywele nyekundu.
Ana nywele za kahawia.
Ana nywele za shaba.
Ana mvi.

16 Sweta yake ni rangi gani?
Sweta yake ni ya buluu.
Suti yako ni rangi gani?
Suti yangu ni ya kijivu.
Nywele zake ni rangi gani?
Nywele zake ni za kahawia.

17 Nywele zake ni rangi gani?
Nywele zake ni za shaba.
Nywele zao ni rangi gani?
Nywele zao ni nyeusi.
Nywele zako ni rangi gani?
Nywele zangu ni nyekundu.

18 Msichana anahisi baridi.
Mvulana anahisi joto.
Mwanamume anahisi baridi.
Mwanamke anahisi joto.

19 Mwanamume ana njaa.
Mvulana ana kiu.
Mwanamke ana njaa.
Msichana ana kiu.

20 Nina njaa.
Nina kiu.
Ninahisi joto.
Ninahisi baridi.

21 Je, una kiu?
Ndiyo, nina kiu.
Je, mnahisi baridi?
Hapana, hatuhisi baridi.
Je, una njaa?
Hapana, sina njaa.
Je, mnahisi joto?
Ndiyo, tunahisi joto.

22 Je, unahisi baridi?
Ndiyo, ninahisi baridi.
Je, mna kiu?
Hapana, hatuna kiu.
Je, unahisi joto?
Hapana, sihisi joto.
Je, mna njaa?
Ndiyo, tuna njaa.

23 Mvulana amechoka.
Msichana ni mgonjwa.
Mwanamume ni mgonjwa.
Mwanamke amechoka.

## 2.4 Inaendelea

24 Je, wewe ni mgonjwa?
Hapana, mimi si mgonjwa.
Je, umechoka?
Hapana, sijachoka.

25 Mimi ni mgonjwa.
Nimechoka.
Ninahisi baridi.
Nina njaa.

26 Hujambo?
Mimi ni mgonjwa.
Hujambo?
Sijambo.

27 Hujambo?
Nimechoka.
Hujambo?
Sijambo.

28 Habari?
Nzuri. Hujambo?
Sijambo.

29 Habari?
Nzuri. Hujambo?
Sijambo.
Habari?
Nzuri. Hamjambo?
Hatujambo.

30 Hamjambo?
Hatujambo.
Kwaherini.
Kwaherini.

31 Hujambo Sara?
Sijambo Bwana Jones.
Hamjambo?
Hatujambo.

32 Hujambo Bi. Jones?
Sijambo.
Kwaheri.
Hujambo Sara?
Sijambo.
Kwaheri.

33 Shikamoo baba.
Marahaba Amy.
Hujambo?
Sijambo.

34 Shikamoo!
Marahaba, jina lako ni nani?
Jina langu ni Bobby Jones.
Nimefurahi kukutana na wewe.
Kwaheri.

35 Shikamoo mama!
Marahaba Amy.
Hujambo?
Mimi ni mgonjwa.
Hujambo?
Sijambo.

36 Shikamoo nyanya.
Marahaba Amy.
Hujambo?
Sijambo.
Hujambo?
Sijambo.

## 2.5 Mazingatio

01 Shikamoo!
Marahaba.

02 Habari?
Nzuri.

03 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Paulo Lima.

04 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Pei-chi Yu.

05 Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

06 Je, huyu ni mdogo wako wa kiume?
Ndiyo, huyu ni mdogo wangu wa kiume.

07 Jina lako ni nani?
Jina langu ni Pei-li.

08 Una umri gani?
Nina umri wa miaka tisa.

09 Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

10 Mnatoka nchi gani?
Tunatoka Uchina.

11 Na wewe unatoka nchi gani?
Ninatoka Brazili.

12 Je, una njaa?
Hapana, sina njaa.

13 Je, una njaa?
Ndiyo, nina njaa.

14 Kwaheri.
Kwaherini.

15 Je, hiki ni kitabu chako?
Ndiyo, hiki ni kitabu changu.

16 Je, hii ni familia yako?
Ndiyo, hii ni familia yangu.

17 Familia yako inaishi wapi?
Familia yangu inaishi Beijing.

18 Je, una kiu?
Ndiyo, nina kiu.

# 3.1 Somo Kuu

01 Wanawake wanafanya kazi.
Wavulana wanacheza.
Mwanamume anafanya kazi.
Msichana anacheza.

02 shule
hospitali
hoteli
bustani

03 Daktari hufanya kazi hospitalini.
Wanaume hufanya kazi katika bustani.
Wanawake hufanya kazi hotelini.
Mwalimu hufanya kazi shuleni.

04 Ninacheza katika bustani.
Ninacheza shuleni.
Ninafanya kazi hospitalini.
Ninafanya kazi shuleni.

05 Familia inakula ndani.
Mwanamume na mwanamke wanakula nje.
Mwanamume anakimbia ndani.
Mwanamke anakimbia nje.

06 Mwanamume huyu hufanya kazi ndani.
Wanaume hawa hufanya kazi nje.
Wanawake hawa hufanya kazi ndani.
Mwanamke huyu hufanya kazi nje.

07 asubuhi
mchana
jioni
usiku
asubuhi
mchana
jioni
usiku

08 Ni asubuhi.
Ni mchana.
Ni jioni.
Ni usiku.

09 Ni asubuhi. Watoto wanapata kifunguakinywa.
Ni mchana. Wanaume wanakula chakula cha mchana.
Ni jioni. Familia inakula chakula cha jioni.

10 Familia inapata kifunguakinywa ndani.
Familia inapata kifunguakinywa nje.
Anakula chakula cha mchana ndani.
Anakula chakula cha mchana nje.

11 Tunapata kifunguakinywa ndani.
Tunakula chakula cha jioni nje.
Tunapata kifunguakinywa nje.
Tunakula chakula cha jioni ndani.

12 Yeye hufanya kazi asubuhi.
Yeye hufanya kazi usiku.
Wao hucheza mchana.
Yeye hutazama televisheni jioni.

13 Wewe hufanya kazi wapi?
Mimi hufanya kazi katika bustani.
Mimi hufanya kazi hospitalini.
Mimi hufanya kazi shuleni.
Mimi hufanya kazi hotelini.

14 Wewe hufanya kazi wakati gani?
Mimi hufanya kazi asubuhi.
Wewe hufanya kazi wakati gani?
Mimi hufanya kazi mchana.
Wewe hufanya kazi wakati gani?
Mimi hufanya kazi usiku.

15 Wewe hunywa kahawa wapi?
Mimi hunywa kahawa shuleni.
Wewe hunywa kahawa wakati gani?
Mimi hunywa kahawa asubuhi.
Wewe hunywa kahawa wakati gani?
Mimi hunywa kahawa jioni.

16 Amevaa viatu na soksi.
Amevaa viatu lakini hajavaa soksi.
Nimevaa suti na tai.
Nimevaa suti lakini sijavaa tai.

17 Ana yai na analila.
Ana yai lakini halili.
Msichana ana kitabu na anakisoma.
Msichana ana kitabu lakini hakisomi.

18 Je, una soksi na viatu?
Nina soksi lakini sina viatu.
Je, una kaka na dada?
Ndiyo, nina kaka wawili na dada wawili.
Je, una koti na kofia?
Nina koti lakini sina kofia.

19 Yeye husoma kabla ya kulala.
Yeye husoma baada ya kula chakula cha mchana.
Yeye hunywa kahawa kabla ya kufanya kazi.
Wao hunywa kahawa baada ya kula chakula cha jioni.

20 Wewe hupata kifunguakinywa wakati gani?
Mimi hupata kifunguakinywa kabla ya kufanya kazi.
Wewe hula chakula cha jioni wakati gani?
Mimi hula chakula cha jioni baada ya kufanya kazi.

21 mayai kumi na tatu
vikombe kumi na nne
tai kumi na tano
mikanda kumi na sita

22 sahani kumi na saba
mipira kumi na nane
maua kumi na tisa
vitabu ishirini

23 kumi na tatu
kumi na nne
kumi na tano
kumi na sita
kumi na saba
kumi na nane
kumi na tisa
ishirini

24 Kumi na nne huja baada ya kumi na tatu.
Kumi na tano huja baada ya kumi na nne.
Kumi na tisa huja kabla ya ishirini.

25 Kumi na tano huja kabla ya kumi na sita.
Kumi na saba huja baada ya kumi na sita.
Kumi na saba huja kabla ya kumi na nane.
Kumi na nne huja baada ya kumi na tatu.

26 Una umri gani?
Nina umri wa miaka kumi na nne.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka kumi na tisa.

27 Habari za asubuhi?
Habari za mchana?
Habari za jioni?
Usiku mwema.

28 Habari za asubuhi?
Nzuri.
Habari za mchana?
Nzuri.

29 Habari za jioni?
Nzuri.
Hujambo?
Sijambo. Na wewe hujambo?
Mimi ninahisi baridi.
Usiku mwema.
Usiku mwema.

30 Habari za asubuhi?
Mimi ni Dan Parker.
Huyu ni Jane Taylor.
Hiki ni kitabu chake.
Hujambo Bi. Taylor?
Sijambo.

31 Wewe huandika wakati gani?
Mimi huandika asubuhi na jioni.
Wewe hufanya nini mchana?
Mimi hucheza na mtoto wangu.

## 3.2 Somo Kuu

01 siku saba
Mtoto huyu mchanga ana umri wa siku moja.
siku mbili
Paka huyu ana umri wa siku ishirini.

02 Kuna siku saba katika wiki.
Kuna wiki nne katika mwezi.
Kuna miezi kumi na mbili katika mwaka.

03 siku
wiki
mwezi
mwaka

04 Ana umri wa siku kumi na nane.
Ana umri wa wiki kumi na nane.
Ana umri wa miezi kumi na nane.
Ana umri wa miaka kumi na nane.

05 Siku hii ni Ijumaa.
Siku hii ni Jumamosi.
Siku hii ni Jumapili.

06 Leo ni Ijumaa. Ninafanya kazi.
Leo ni Jumamosi. Ninakimbia.
Leo ni Jumapili. Ninatazama televisheni.

07 Leo ni Jumapili. Wanatembea katika bustani.
Leo ni Jumatatu. Tunakula chakula cha mchana.
Leo ni Jumanne. Ninanunua samaki.

08 Leo ni Jumatano. Ninasoma.
Leo ni Alhamisi. Ninasikiliza redio.
Leo ni Ijumaa. Wanacheza.
Leo ni Jumamosi. Anaogelea.

09 Jumatatu
Jumanne
Jumatano
Alhamisi
Ijumaa
Jumamosi
Jumapili

10 Jumatatu
Jumanne
Jumatano
Alhamisi
Ijumaa
Jumamosi
Jumapili

11 Wanacheza na watoto wao.
Msichana anakula na rafiki zake.
Msichana anasoma na babu yake.
Mvulana anaogelea na rafiki zake.

12 Unakula chakula cha mchana na nani?
Ninakula chakula cha mchana na mdogo wangu wa kike.
Unakula chakula cha jioni na nani?
Ninakula chakula cha jioni na mume wangu.

13 Mvulana anamtembelea nyanya yake.
Msichana anamtembelea rafiki yake.
Mwanamke anatalii Paris.
Mwanamume anatalii Mosko.

14 Unafanya nini?
Ninacheza na dada yangu.
Unafanya nini?
Ninamtembelea nyanya yangu hospitalini.

15 Ninawatembelea rafiki zangu.
Familia inatalii Roma.
Mume na mke wanatalii Beijing.
Mvulana anamtembelea babu yake.

16 Familia inatalii New York.
Wanawake wanatalii Japani.
Anawatembelea wazazi wake.
Tunamtembelea babu yetu.

17 Hii ni familia yangu.
Hii ni nyumba yetu.
Hawa ni wageni wetu.
Hii ni familia yangu.
Hii ni nyumba yetu.
Hawa ni wageni wetu.

18 Wao ni wageni.
Ninafanya kazi. Mimi si mgeni.
Yeye ni mgeni.

19 Wageni wetu wapo mlangoni.
Wageni wetu wamekaa sebuleni.
Tunakula chakula cha jioni na wageni wetu.
Tunacheza na wageni wetu.

20 Asante.
Karibu.
Asante.
Karibu.

21 Asante.
Karibu.
Asante.
Karibu.

22 Asante.
Karibu.

23 Karibu nyumbani kwetu.
Karibu hotelini kwetu.
Karibu Tanzania.

24 Karibuni hotelini kwetu.
Asante.
Karibuni nyumbani kwetu.
Asante.

25 Habari?
Nzuri.
Unatoka nchi gani?
Ninatoka Urusi.
Karibu Kenya.
Asante.

26 Wageni wetu wapo mlangoni.
Habari?
Karibuni nyumbani kwetu.
Asante.

27 Mwanamke ananusa kahawa.
Mwanamume ananusa ua.
Mwanamke anaonja wali.
Wanaonja mkate.

28 Mkate ni mtamu.
Maziwa si matamu.
Maua yananukia vizuri.
Soksi zinanuka vibaya.

29 Mwanamke anaonja mkate.
Tofaa ni tamu.
Kahawa si tamu.
Mwanamume ananusa maziwa.
Ua linanukia vizuri.
Samaki ananuka vibaya.

30 Mwanamume ananusa maziwa.
Maziwa yananuka vibaya.
Wanaonja wali.
Wali ni mtamu.

31 Hii inanuka vibaya.
Hii inanukia vizuri.
Hii si tamu.
Hii ni tamu.

32 vidole vinne
mikono mitatu
vidole kumi vya miguu
mguu mmoja

33 mkono
vidole
mguu
vidole vya mguu

34 Mguu wake uko nyasini.
Vidole vyake vya miguu vimo majini.
Mikono yake iko dirishani.
Vidole vyake viko mezani.

35 nyumba katika majira ya barafu
bustani katika majira ya kuchipua majani
jiji katika majira ya joto
mti katika majira ya kudondoka majani

36 majira ya kuchipua majani
majira ya joto
majira ya kudondoka majani
majira ya barafu

## 3.2 Inaendelea

37 Huu ni mti katika majira ya barafu.
Huu ni mti katika majira ya kuchipua majani.
Huu ni mti katika majira ya joto.
Huu ni mti katika majira ya kudondoka majani.

38 Hii ni nyumba yangu katika majira ya barafu.
Hii ni nyumba yangu katika majira ya joto.
Hii ni kofia yangu katika majira ya barafu.
Hii ni kofia yangu katika majira ya joto.

39 Jina langu ni Yusuf Kimani. Jina lako ni nani?
Jina langu ni Michael Levy.
Nimefurahi kukutana na wewe.

40 Habari za mchana?
Nzuri.

41 Wewe huishi wapi?
Mimi huishi kwenye nyumba nyekundu.
Wewe hufanya kazi wapi?
Mimi hufanya kazi hotelini.
Wewe hufanya kazi siku gani?
Mimi hufanya kazi Jumatatu, Jumanne na Alhamisi.

42 Habari za asubuhi?
Nzuri.
Mtoto wako mchanga ana umri gani?
Mtoto wangu mchanga ana umri wa wiki tisa.
Mtoto wako wa kiume ana umri gani?
Mtoto wangu wa kiume ana umri wa miezi kumi na nane.

## 3.3 Somo Kuu

01 Mwanamume huyu anaandika.
Mwanamke huyu anasoma.
Mwanamume huyu anaongea.
Mwanamke huyu anaongea.

02 Mwanamume anasoma Kichina.
Mwanamke anasoma Kiingereza.
Mvulana anaandika Kiarabu.
Msichana anaandika Kiswahili.

03 Anaandika Kiarabu.
Anasoma Kiarabu.
Anaongea Kiarabu.
Anaandika Kichina.
Anasoma Kichina.
Anaongea Kichina.

04 Msichana anaongea Kiingereza.
Mvulana anaongea Kiswahili.
Mwanamume anaongea Kiingereza.
Mwanamke anaongea Kiswahili.

05 Anaandika Kiswahili.
Anasoma Kiswahili.
Anaongea Kiswahili.

06 Ninasoma Kichina.
Ninaandika Kichina.
Ninasoma Kiswahili.
Ninaandika Kiswahili.

07 Mwanamume huyu anatoka Australia.
Mwanamke huyu anatoka Urusi.
Msichana huyu anatoka Japani.
Mvulana huyu anatoka Kenya.

08 Mbwa, paka na farasi ni wanyama.
Wanaume, wanawake, wasichana na wavulana ni watu.

09 Huyu ni mnyama.
Huyu ni mtu.
Hawa ni wanyama.
Hawa ni watu.

10 Watu wa Misri huongea Kiarabu.
Watu wa Uchina huongea Kichina.
Watu wa Tanzania huongea Kiswahili.
Watu wa Australia huongea Kiingereza.

11 Mtu huyu anatoka Uchina. Yeye huongea Kichina.
Mnyama huyu anatoka Uchina. Haongei Kichina.
Mtu huyu anatoka Australia. Yeye huongea Kiingereza.
Mnyama huyu anatoka Australia. Haongei Kiingereza.

12 Wanawake wanatoka Japani.
Wao huongea Kijapani.
Wanaume wanatoka Kenya.
Wao huongea Kiswahili.
Ninatoka Marekani.
Mimi huongea Kiingereza.

13 Je, wewe huongea Kiingereza?
Ndiyo, mimi huongea Kiingereza.
Je, wewe huongea Kiswahili?
Ndiyo, mimi huongea Kiswahili.
Je, wewe huongea Kijapani?
Ndiyo, mimi huongea Kijapani.

14 Je, wewe huongea Kiswahili?
Hapana, siongei Kiswahili.
Je, wewe huongea Kiswahili?
Ndiyo, mimi huongea Kiswahili.

15 Samahani.
Je, wewe huongea Kiswahili?
Hapana, siongei Kiswahili.
Je, wewe huongea Kiingereza?
Ndiyo, mimi huongea Kiingereza.

16 Samahani.
Je, wewe huongea Kiingereza?
Hapana, siongei Kiingereza.
Samahani.
Je, wewe huongea Kiingereza?
Ndiyo, mimi huongea Kiingereza.

17 mikanda kumi
vikombe ishirini
mipira thelathini
sahani arobaini
tai hamsini
kofia sitini

18 kumi
ishirini
thelathini
arobaini
hamsini
sitini

19 vikombe ishirini
vikombe ishirini na moja
vikombe ishirini na mbili
sahani ishirini na tatu
sahani ishirini na nne
sahani ishirini na tano

20 mabakuli thelathini na nne
mabakuli thelathini na tano
mabakuli thelathini na sita
sahani thelathini na saba
sahani thelathini na nane
sahani thelathini na tisa

21 arobaini na nne
arobaini na tano
arobaini na sita
arobaini na saba
arobaini na nane
arobaini na tisa

22 arobaini
arobaini na moja
arobaini na mbili
arobaini na tatu
arobaini na nne
arobaini na tano
arobaini na sita
arobaini na saba
arobaini na nane
arobaini na tisa

## 3.3 Inaendelea

23 kumi
ishirini
thelathini
arobaini
hamsini
sitini

24 Una umri gani?
Nina umri wa miaka arobaini na tano.
Ana umri gani?
Ana umri wa miaka thelathini.
Una umri gani?
Nina umri wa miaka thelathini na tano.

25 Tuna sahani ngapi?
Tuna ishirini na nne.
Tuna mabakuli mangapi?
Tuna arobaini na tano.
Kuna wageni wangapi?
Kuna thelathini.

26 Ninafundisha Kiingereza.
Anafundisha Kiarabu.
Anafundisha Kichina.
Je, unafundisha Kiswahili?

27 Anawafundisha wavulana Kiarabu.
Anawafundisha wavulana Kiingereza.
Anawafundisha wasichana Kichina.
Anawafundisha wasichana Kiswahili.

28 Ninajifunza Kichina.
Anajifunza Kiarabu.
Wanajifunza Kiingereza.
Tunajifunza Kiswahili.

29 Ninafundisha Kiingereza.
Unajifunza Kiingereza.
Unafundisha Kiarabu.
Tunajifunza Kiarabu.

30 Mwalimu wako ni nani?
Mwalimu wangu ni Bi. Li.
Mwalimu wako ni nani?
Mwalimu wangu ni Bwana Haddad.

31 Ninafundisha Kichina.
Tunajifunza Kichina.
Ninafundisha Kiswahili.
Ninajifunza Kiswahili.

32 Jina langu ni Reem.
Mimi huongea Kiarabu lakini ninajifunza Kiingereza.
Huyu ni mwalimu wangu. Jina lake ni Bwana Haddad.

33 Jina langu ni Lin.
Wazazi wangu wanatoka Uchina.
Tunaishi New York.
Wazazi wangu hawaongei Kiingereza.
Mimi huongea Kiingereza na Kichina.
Ninajifunza Kiswahili.

## 3.4 Somo Kuu

01 Mvulana ameamka.
Mume anamwamsha mke wake.
Mwanamume anamwamsha rafiki yake.
Msichana ameamka.

02 Mvulana ameamka.
Mwanamke ameamka.
Msichana ameamka.
Mwanamume ameamka.

03 Mwanamke anamwamsha msichana.
Mwanamke ameamka.
Mwanamume ameamka.
Mwanamume anamwamsha mvulana.

04 Anaosha vikombe.
Anafua soksi.
Ninafua shati.
Anaosha gari.

05 Ninaosha bakuli.
Wanafua soksi.
Unafua sweta!
Anaosha sahani.

06 Wanaosha sahani.
Wanaosha gari lao.
Anafua sketi yake.
Anafua fulana yake.

07 Msichana ananawa uso wake.
Mwanamke ananawa uso wake.
Nyuso zao ni za zambarau na manjano.

08 Ninanawa mikono yangu.
Mwanamke anaosha nywele zake.
Mwanamume ananawa uso wake.

09 Mpira uko mguuni kwake.
Mpira uko kidoleni kwake.
Mpira uko usoni kwake.

10 Barabara imeloa.
Fulana ni kavu.
Mbwa wameloa.
Paka ni mkavu.

11 Farasi wameloa.
Farasi ni wakavu.
Nywele zake zimeloa.
Nywele zake ni kavu.

12 Soksi ni chafu.
Shati ni safi.
Uso wa msichana ni mchafu.
Uso wa mwanamume ni msafi.

13 Shati ni chafu.
Shati limeloa.
Shati ni safi na kavu.

14 Mama yuko wapi?
Yumo bafuni.
Baba yuko wapi?
Yumo jikoni.

15 Kwa nini unanawa mikono yako?
Ninanawa mikono yangu kwa sababu ni michafu.
Kwa nini umevaa sweta?
Nimevaa sweta kwa sababu ninahisi baridi.

16 Kwa nini baba yumo jikoni?
Baba yumo jikoni kwa sababu anapika.
Kwa nini mama anamwosha mbwa?
Mama anamwosha mbwa kwa sababu ni mchafu.
Kwa nini unakunywa maji?
Ninakunywa maji kwa sababu nina kiu.

17 Kwa nini umo bafuni?
Nimo bafuni kwa sababu ninanawa mikono yangu.
Kwa nini unanawa mikono yako?
Ninanawa mikono yangu kwa sababu ni michafu.

18 mswaki
mswaki
mswaki
dawa ya meno
dawa ya meno
meno

# 3.4 Inaendelea

19 brashi
brashi
brashi
sabuni
sabuni
taulo

20 mswaki
dawa ya meno
meno
brashi
sabuni
taulo

21 Mwanamke anachana nywele zake.
Mwanamume anapiga mswaki.
Wasichana wanachana nywele zao.
Wavulana wanapiga mswaki.

22 Ninapiga mswaki.
Anachana nywele zake.
Wananawa mikono yao.
Anapiga mswaki.

23 Anaosha nywele zake.
Anachana nywele zake.
Anaosha nywele zake.
Anachana nywele zake.

24 Ananunua brashi.
Wananawa mikono yao kwa sabuni.
Ninapiga mswaki.

25 Mama anamwamsha binti yake.
Binti anachana nywele zake.
Kaka yake anapiga mswaki.
Baba ananawa uso wake.

26 Mimi hunawa mikono yangu kabla ya chakula cha mchana.
Mimi hupiga mswaki baada ya kifunguakinywa.
Mimi hunywa kahawa baada ya chakula cha jioni.
Mimi huchana nywele zangu kabla ya kifunguakinywa.

27 mto
mto
mto
shuka
shuka
blanketi

28 shuka
mto
blanketi
taulo

29 Shuka ipo kitandani.
Paka yupo juu ya mto.
Taulo imo bafuni.

30 Shuka ya pinki ni safi.
Mto wa pinki ni msafi.
Blanketi la pinki ni safi.
Taulo ya pinki ni safi.

31 Kwa nini mbwa ananuka vibaya?
Kwa sababu ni mchafu na ameloa.
Kwa nini shuka zinanukia vizuri?
Kwa sababu ni safi.

32 Kwa nini watu wamo katika chumba cha maakuli?
Kwa sababu wanakula chakula cha jioni.
Kwa nini watu wamo jikoni?
Kwa sababu wanaosha mabakuli na sahani zao.
Kwa nini watu wamo sebuleni?
Kwa sababu wanatazama televisheni.

33 Wazazi wanasoma sebuleni.
Mwanamke amelala katika chumba cha kulala.
Msichana anasoma katika chumba cha kulala.
Mvulana amelala sebuleni.

34 Unanunua nini?
Ninanunua maua.
Unanunua maua mangapi?
Ninanunua maua tisa.
Kwa nini unanunua maua?
Ninanunua maua kwa sababu nyanya yangu ni mgonjwa.
Nyanya yako huishi wapi?
Yeye huishi New York.

## 3.5 Mazingatio

01 Habari Jane?
Nzuri.

02 Una mabakuli mangapi?
Nina mabakuli mawili.

03 Je, kinanukia vizuri?
Ndiyo, kinanukia vizuri.

04 Je, ni kitamu?
Ndiyo, ni kitamu.

05 Hii ni nini?
Huu ni wali.

06 Habari?
Nzuri.

07 Habari?
Nzuri.

08 Hujambo?
Sijambo.

09 Huyu ni rafiki yangu. Jina lake ni Anna.
Anatoka Urusi.

10 Je, wewe huongea Kiswahili?
Ndiyo, mimi huongea Kiswahili.

11 Nimefurahi kukutana na wewe.
Nimefurahi kukutana na wewe pia.

12 Wewe hufanya kazi wapi?
Mimi hufanya kazi shuleni.

13 Na wewe hufanya kazi wapi?
Mimi hufanya kazi hospitalini.

14 Je, wewe hucheza?
Ndiyo, mimi hucheza.

15 Je, na wewe hucheza?
Ndiyo, mimi hucheza.

16 Wewe hucheza wakati gani?
Mimi hucheza jioni baada ya kazi.

17 Wewe hucheza wapi?
Mimi hucheza katika bustani.

18 Kwaheri.
Kwaheri.

19 Kwaheri.
Kwaheri.

20 Uko wapi?
Nimo jikoni.

21 Unafanya nini?
Ninaosha sahani.

22 Kwa nini unaosha sahani?
Ninaosha sahani kwa sababu mimi ni rafiki yako.

# 4.1 Somo Kuu

01 Wanawake hawa wana miavuli.
Mwanamume huyu ana tiketi.
Mwanamke huyu ana miwani ya jua.
Wanaume hawa wana ngazi.

02 mwavuli
tiketi
miwani ya jua
ngazi

03 Anahitaji ngazi.
Anahitaji taulo.
Anahitaji sabuni.
Anahitaji miwani ya jua.

04 Anahitaji fedha.
Ana fedha.
Fedha ziko mezani.

05 Anahitaji fedha.
Ana fedha.
Anahitaji mwavuli.
Ana mwavuli.

06 Nina miwani ya jua.
Ninahitaji miwani ya jua.
Una tiketi.
Unahitaji tiketi.

07 Je, unahitaji funguo?
Ndiyo, ninahitaji funguo.
Je, unahitaji fedha?
Ndiyo, ninahitaji fedha.

08 vito
vito
vito
nguo
nguo
toi

09 matunda
matunda
matunda
mboga
mboga
nyama

10 nyama
mboga
matunda
toi
nguo
vito

11 Wananunua nyama.
Ananunua nguo.
Ananunua toi.
Wananunua mboga.

12 Nyumba nyeupe ni ya zamani.
Gari la kijani ni jipya.
Nyumba nyekundu ni mpya.
Gari la buluu ni la zamani.

13 televisheni ya zamani
televisheni mpya
simu ya zamani
simu mpya

14 Yeye huuza suti.
Ananunua suti.
Yeye huuza mashati.
Ananunua shati.

15 Sisi huuza mikate.
Sisi huuza maua.
Sisi huuza baiskeli.

16 Yeye huuza viatu.
Ananunua viatu.
